

TANGAZO LA SERIKALI NA. LA TAREHE

**SHERIA YA SERIKALI ZA MITAA (MAMLAKA ZA MIJI)
(SURA YA 288)**

SHERIA NDOGO

Zimetungwa chini ya kifungu cha 89

**SHERIA NDOGO ZA (ADA YA MAENDELEO YA ELIMU) ZA HALMASHAURI
YA MANISPAA YA LINDI YA 2014**

Jina na mwanzo wa kutumika	1	Sheria Ndogo hizi zitaitwa Sheria Ndogo za (Ada ya Maendeleo ya Elimu) za Halmashauri ya Manispaa ya Lindi za mwaka 2014 na zitaanza kutumika baada ya kutangazwa kwenye Gazeti la Serikali.
Eneo la matumizi	2	Sheria Ndogo hizi zitatumika katika eneo lote la Mamlaka ya Halmashauri ya Manispaa ya Lindi.
Tafsiri	3	<p>Katika Sheria Ndogo hizi isipokuwa itakapoelezwa vinginevyo:-</p> <p>“Halmashauri” maana yake ni Halmashauri ya Manispaa ya Lindi,</p> <p>“<i>Kampuni</i>” maana yake ni kampuni, yoyote iliyosajiriwa kwa mujibu wa Sheria za Nchi inayofanya biashara katika Halmashauri ya Manispaa ya Lindi, bila kujali kama kampuni hiyo ina makazi au la.</p> <p>“<i>Kaya</i>” maana yake ni baba, mama na watoto chini ya miaka kumi na nane, mtu yeyote yule mwenye umri zaidi ya miaka 18 anayejitegemea.</p> <p>“<i>Mkazi</i>” maana yake ni mtu yeyote yule mwenye uwezo wa kufanya kazi anayeishi, au kufanya shughuli zake ndani ya eneo la mamlaka ya Halmashauri ya Manispaa ya Lindi,</p> <p>“<i>Mkurugenzi</i>” maana yake ni Mkurugenzi wa Halmashauri ya Manispaa ya Lindi,</p>

“*Mtu*” maana yake ni mkazi, taasisi ya fedha, kampuni, taasisi za umma, vyama vya ushirika na vyama vya msingi.

“*Taasisi za Fedha*” maana yake ni kampuni yeyote ile inayoshughulika na shughuli za kibenki, ikiwa ni pamoja na kutoa mikopo,

Wajibu wa kulipa Ada ya maendeleo ya Elimu	4	<ol style="list-style-type: none">(1) Kutakuwa na ada ya Maendeleo ya Elimu katika Halmashauri itakayolipwa na kila mkazi, kaya, taasisi, kampuni kama itakavyoainishwa katika jedwali la Sheria Ndogo hizi.(2) Ada hiyo italipwa mara moja kwa mwaka.(3) Itakuwa ni jukumu la kila mwajiri katika Halmashauri kukusanya Ada ya Maendeleo ya Elimu kutoka kwa Waajiriwa wake na kuwasilisha kwa Mkurugenzi.(4) Mwisho wa kulipa Ada ya Maendeleo ya Elimu bila adhabu isipokuwa kwa kampuni zinazojishughulisha na ununuzi wa mazao itakuwa ni mwezi Septemba.(5) Bila ya kuathiri kifungu kidogo cha (4), mwisho wa kulipa Ada ya Maendeleo ya Elimu kwa makampuni yanayojihusisha na ununuzi wa mazao na vyama vya msingi itakuwa ni baada ya msimu wa zao husika kufungwa
Adhabu	5	Mtu teyote atakayekwenda kinyume na Sheria Ndogo hizi atakuwa ametenda kosa na akipatikana na hatia atatozwa faini isiyozidi Shilingi elfu hamsini (50,000) au kifungo cha miezi kumi na mbili au vyote kwa pamoja yaani faini na kifungo.
Kufifilisha kosa	6	Mkurugenzi anaweza kufifilisha kosa kwa mujibu wa Sheria Ndogo hizi, iwapo mkosaji atakuwa amekiri kwa maandishi ambapo mkosaji atalazimika kulipa ada anayodaiwia pamoja na faini isiyozidi Shilingi Elfu Arobaini (40,000/=) tu.

JEDWALI LA KWANZA

Chini ya Kifungu cha 4(1)

Na.	Mlipaji	Kiwango
1.	Kaya	Shilingi 3,000/= kwa mwaka
2.	Waajiriwa	3% ya mshahara wake wa mwezi mmoja kwa mwaka. Iwapo 3% ya mshahara ni chini ya Shilingi 3,000/= atalipa Shilingi 3,000/=
3.	Benki	Shilingi 1,000,000/= kwa mwaka.
4.	Taasisi za Pesa zinazokopesha tu (Faidika, Bayport, n.k.)	Shilingi 500,000/= kwa mwaka
5.	Vyama vya Msingi	Shilingi 1,000,000/= kwa mwaka
6.	Chama Kikuu cha Ushirika	Shilingi 3,000,000/= kwa mwaka
7.	Wanunuzi wa Mazao	Shilingi 3/= kwa kila kilo wanayonunua.
8.	Ushuru wa mazao	Shilingi 1/= kwa kilo.
9.	Madiwani	Shilingi 50,000/= kwa mwaka
10.	Wabunge	Shilingi 500,000/= kwa mwaka
11.	Mashirika ya Umma na binafsi	Shilingi 1,000,000/= kwa mwaka
12.	Kampuni za Ukandarasi	Shilingi 500,000/= kwa mwaka
13.	Wazabuni wa Halmashauri	Shilingi 200,000/= kwa mwaka
14.	Wafanya biashara :- (a) Jumla (b) Wakubwa (c) Wadogo	Shilingi 100,000/= kwa mwaka Shilingi 50,000/= kwa mwaka Shilingi 20,000/= kwa mwaka
15.	Kampuni za kibiashara	Shilingi 1,000,000/= kwa mwaka

JEDWALI LA PILI

(Chini ya kifungu cha 6)

FOMU YA KUFIFILISHA KOSA

Mimi..... wa S.L.P.
..... ninayefanya biashara ya
..... lililopo ndani ya Halmashauri ya Manispaa ya Lindi – kifungu cha
..... cha Sheria Ndogo za Ada ya Maendeleo ya Elimu) za
Halmashauri ya Manispaa ya Lindi za mwaka 2014. Kwa hiyo, kwa hiari yangu mwenyewe na bila
kushawishiwa na mtu yeyote, nakubali kulipa faini iliyoainishwa kwenye Sheria Ndogo hizi iwapo
Mkurugenzi atatekeleza madaraka aliyopewa chini ya kifungu cha 6 cha Sheria Ndogo hizi.

Saini

Mbele yangu (jina)

Saini

Wadhifa